# Dart yatoa msimamo mwendokasi kurejea Kibaha

Nasra Abdalah, Mwananchio
nabdalah@mwananchi.co.tz


Huduma ya usafiri wa mabasi ya mwendokasi imerejea rasmi kutoka Kibaha hadi Kimara.

**Dar es Salaam.** Wakati Kampuni ya Mabasi yaendayo Haraka (Udart), ikisubiri majibu ya Wakala wa Mabasi hayo (Dart), kutoa kibali kurejesha huduma za mabasi hayo wilayani Kibaha mkoani Pwani, yenyewe imetoa msimamo wake.

Dart wanakuja na msimamo huo ikiwa imepita miaka miwili tangu huduma hizo zisitishwe, ambapo Udart walitoa sababu nne zilizosababisha hayo, ikiwamo kusubiri kibali kutoka Dart.

Akizungumza na Mwananchi Digital, wiki mbili zilizopita, Mkurugenzi Mkuu wa Udart, Pius Ng'ingo, aliyataja mambo ambayo yalisitisha huduma hizo kuwa ni pamoja na kukosa vituo kwa ajili ya magari hayo, vibanda vya kukatishia tiketi, ufungwaji wa mashine kwenye magari na suala la nauli.

Ng'ingo alisema kwa kuwa yote hayo yanahusisha taasisi mbalimbali, mengi yapo katika mchakato wa kushughulikiwa baada ya wadau hao kufanya vikao mbalimbali na yatakapokuwa tayari usafiri huo utarejea tena kama kawaida na itakuwa baada ya Wakala wa Usafiri wa Mabasi yaendayo Haraka (Dart) kubariki yote.

Aliongeza kuwa matarajio yao pia ni watakaporejea kutoa huduma hiyo, kuwe na magari yanayotoka moja kwa moja Kibaha hadi Kariakoo au Kibaha hadi Kivukoni, badala ya abiria kupaswa kuunga usafiri huo Kimara Mwisho.

Hata hivyo, wakati Udart wakiwa wanasubiri kibali hicho, Dart kupitia Mtendaji Mkuu wake, Said Tunda, alisema hawawezi kuruhusu

**Sh2,000**

Kiwango cha nauli kilichotangazwa na halmashauri Julai 7, 2026.

hilo kwa kuwa wakala huo kisheria umeanzishwa kutoa huduma katika Mkoa wa Dar es Salaam pekee.

"Unajua Dart maana yake nini ni 'Dar es Salaam Rapid Transit', je, Kibaha ni Dar es Salaam?

"Vituo vyake vikubwa vipo wapi? Mbagala, Kimara, Gongo la Mboto, Tegeta, huko kote ni wapi? Si Dar es Salaam? Huko kwingine hatuna miundombinu ya Dart na sisi kazi yetu ni kusimamia miundombinu hiyo, hivyo nachelea kusema kitu ambacho sina mamlaka nacho," alisema Tunda.

Aidha, Mtendaji huyo alisema huwezi kwenda kwa mke wa jirani eti kwa sababu anakupendeza sana, hapana jamani kuna mipaka. Kama anataka kufanya kazi na huko ataomba kibali kwa Latra kwa kuwa hawa ndio wanafanya kazi na mabasi ya mikoani, pia yanayopita nje ya mfumo wa BRT.

Pia, Tunda alisema ikumbukwe magari si ya Dart ni ya Udart, na kueleza labda wameamua wenyewe kujitanua kwenda huko kwa kuona wataongeza wateja.

Alipoulizwa awali ilikuwaje huduma hizo zikatolewa, Mtendaji huyo alitaka swali hilo waulizwe Udart, na kuhusu sasa kurejea Tunda aliuliza, "Kwani unaona wanaendelea?"

"Sisi mwisho wetu wa kufanya kazi ni Dar es Salaam, akienda huko Pwani atakumbana na Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (Latra)," alifafanua Mtendaji huyo.

Mwananchi juzi, iliwarudia Udart kuwauliza kuhusu mpango wao huo, ambapo msemaji wao, Gabriel Katanga, alisema mpango upo palepale na kueleza kuna baadhi ya vitu bado havijakamilika ikiwamo vituo na vingine hakuwa tayari kuviweka wazi.

Kwa mujibu wa Katanga, huduma hizo zinatarajiwa kuanza sambamba na zile za kwenda Morocco, Kinondoni ambazo zilisitishwa kutokana na ujenzi wa daraja maeneo ya Kinondoni Mkwajuni.

Sakata la kurejeshwa mwendokasi lilipoanzia, Halmashauri ya Kibaha ilitoa tangazo kuwa usafiri huo ungerejea Julai 7, 2026, likibainisha nauli itakuwa ni Sh2,000.

Alipotafutwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo alikiri kuwa ni wao wamelitoa baada ya kukamilisha majadiliano na mtoa huduma na kueleza wakazi wa huko wamekuwa na uhitaji.

Zulfa Chande, mkazi wa Kibaha alisema kama uhitaji upo wa huduma, hiyo ni biashara nzuri na kushauri Serikali iangalie namna inaweza kubadili sheria ya wakala huo.

Mchambuzi wa masuala ya uchumi na kijamii, Oscar Mkude ameunga mkono sheria ya kuanzishwa kwa wakala huo wa Dart.

Hata hivyo, amekuwa tofauti katika utoaji huduma na kueleza foleni za Dar es Salaam zinatokea pembezoni mwa mji, na kutolea mfano Kimara inatokea Kibamba, Kiluvya na Kibaha, huku ile ya Tegeta ikitokea Bunju hadi Bagamoyo, wakati ya Mbagala inatengenezwa kutokea Tua Ngoma hadi Mkuranga.

MAZOEA

# Hatari ya madereva kuwakabidhi usukani wasio na sifa ya udereva

Devotha Kihwelo, Mwananchi
dkihwelo@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Tabia ya baadhi ya madereva wa daladala na malori kuwakabidhi magari watu wasiokuwa na taaluma, leseni au uzoefu wa kutosha wa kuendesha magari ya biashara ni changamoto inayotishia usalama wa abiria na watumiaji wengine wa barabara

Baadhi ya madereva maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakifanya hivyo kwa sababu mbalimbali ikiwamo kwenda kupata chakula, kupumzika wakati wa safari ndefu au kuwapa nafasi wasaidizi wao kujifunza kazi kama njia ya kusaidiana.

Dereva wa daladala anayefanya safari za Mnazi Mmoja hadi Kimanga, jijini Dar es Salaam, Abdul Semeni alikiri tabia ya madereva kuwaachia makondakta au vijana wa kijiweni kuendesha gari kwa muda mfupi, hasa wanapokwenda kula ili wasipoteze muda wa kuwatafuta abiria.

Alisema wakati mwingine dereva na kondakta hufanya hivyo wakiamini wanasaidiana, lakini wanatambua kitendo hicho kinaweza kuwa hatari iwapo mtu anayeendesha hana uwezo wa kumudu gari.

"Ni kweli jambo hili lipo wakati mwingine dereva anaenda kula, halafu anamwachia kondakta au mpiga debe asogeze gari au kulijazia abiria akirudi anakuta gari lipo tayari kuondoka kwa msaada huo, hivyo wakishuka wanapewa Sh1,000 kwa kila mmoja japokuwa tunajua sio utaratibu," alisema.

> "Ni kweli jambo hili lipo wakati mwingine dereva anaenda kula, halafu anamwachia kondakta au mpigadebe asogeze gari au kulijazia abiria akirudi anakuta gari lipo tayari kuondoka kwa msaada huo, hivyo wakishuka wanapewa Sh1,000 kwa kila mmoja japokuwa tunajua sio utaratibu." Abdul Semeni

Naibu Katibu wa Taasisi ya Taaluma ya Madereva Tanzania, Muhidini Sangoti alisema wanafuatilia kwa karibu matukio ya aina hiyo pamoja na changamoto nyingine zinazochangia ajali barabarani na kuendelea kusisitiza umuhimu wa mafunzo rasmi kwa madereva wote wa magari ya biashara.

Alisema bado kuna maeneo ya vijijini ambako ufuatiliaji haujafika kwa kiwango kikubwa, hivyo taasisi hiyo inaendelea kujitanua ili kuhakikisha usimamizi wa taaluma ya udereva unafika katika maeneo yote ya nchi.

"Elimu ni muhimu katika taaluma hii zamani watu wengi walijifunza kuendesha magari barabarani, lakini sasa tunasisitiza mafunzo sahihi ili kupunguza ajali," alisema Sangito.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 24(1) cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 ya mwaka 1973 na marekebisho yake ya mwaka 2023 hakuna mtu anayepaswa kuendesha gari barabarani isipokuwa awe na leseni halali ya udereva.

Aidha, Kifungu cha 24(2) cha sheria hiyo kinakataza mmiliki wa gari au mtu mwenye mamlaka juu ya gari kumruhusu mtu kuendesha chombo hicho iwapo hana leseni halali ya daraja linalohusika.

Masharti hayo yanaweka wajibu wa kisheria kwa mmiliki wa gari na dereva anayesimamia gari kuhakikisha chombo cha moto hakikabidhiwi kwa mtu asiye na sifa zinazotakiwa.

**Darcoboa wakumbusha madereva**

Katibu wa Chama cha Wamiliki wa Daladala Mkoa wa Dar es Salaam (Darcoboa ), Shifwaya Lema alisema si utaratibu wa waajiri au wamiliki wa daladala kuwaajiri watu wasiokuwa madereva, bali tatizo hutokea pale baadhi ya madereva wanapowakabidhi gari marafiki zao, makondakta au wasaidizi wao bila ridhaa ya mwajiri.

"Mmiliki wa gari anapohitaji dereva humtafuta mtu mwenye sifa na kumwajiri hawezi kumwajiri mtu anayejua si dereva, lakini kinachotokea ni baadhi ya madereva wanawaachia wenzao au makondakta waendeshe magari kwa kisingizio cha kwenda kula au kufanya shughuli nyingine huu si utaratibu mzuri na ni kosa," alisema Lema.

Lema alisema baadhi ya madereva hufanya makosa hayo kutokana na kutokujua sheria au kupuuza wajibu wao, dereva anayejitambua hawezi kuondoka na kumwachia mtu mwingine aendeshe gari alilokabidhiwa au kiti chake cha ofisi kirahisi.

"Rai yangu kwa madereva ni kuheshimu kazi yao na kuzingatia sheria za usalama barabarani. Wasimruhusu kila mtu kuendesha gari walilokabidhiwa, kwa sababu kazi ya udereva ni taaluma yenye wajibu mkubwa wa kulinda maisha ya watu," alisema.

**Uzoefu kazini ni muhimu**

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (Tamstoa), Chuki Shaban alisema suluhisho la kupata madereva bora si kuwazuia wasiokuwa na sifa ambao ni wasaidizi wa madereva na kuwaamini ambao wamepita darasani bali elimu kwa vitendo ndiyo muhimu zaidi.

Alisema kujenga uzoefu kwa vitendo hakumaanishi kuruhusu watu wasiokuwa na sifa au taaluma kuendesha malori wakiwa na mizigo au abiria, bali ni kuwapa nafasi ya kujifunza chini ya uangalizi wa dereva mwenye uzoefu na anayekidhi vigezo vya kisheria ili kulinda usalama wa watumiaji wa barabara.

"Wapo madereva wamesoma na wana leseni lakini wakipewa magari ya masafa marefu wanatetemeka na kuwa chanzo cha ajali wakati aliyejifunza kupitia kwa dereva bila kuingia darasani anaweza kumudu bila kusababisha ajali," alisema Shaban.

Alisema anaamini katika kujenga uzoefu kwa vitendo kwani mtu anaweza kumaliza chuo na kujifunza kuendesha, lakini bado anahitaji kuambatana na dereva mwenye uzoefu ili ajifunze mazingira halisi ya kazi.

**Polisi waonya**

Mrakibu Msaidizi wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani makao makuu, Dumu Mwalugenge alisema kumkabidhi mtu chombo cha moto asiye na sifa, leseni au mafunzo ya udereva ni kosa linaloweza kuwafanya wahusika kuwajibishwa kisheria endapo ajali itatokea.

"Kumpa mtu asiye na sifa chombo chochote cha moto ni kosa, ajali ikitokea uchunguzi utafanyika na wote wanaohusika watachukuliwa hatua na kama kuna makosa suala linaweza kufikishwa mahakamani," alisema Mwalugenge.

Alisema uzoefu pekee wa kuendesha gari hauondoi umuhimu wa kuwa na leseni halali na sifa zinazotakiwa kisheria, kwani mtu anaweza kuonekana anajua kuendesha lakini bado akawa amekiuka sheria.

Alitoa wito kwa wananchi kutoa taarifa wanapoona dereva akifanya vitendo vinavyoashiria kutokuwa na uwezo, ikiwamo kushindwa kutumia breki vizuri, kuyumba barabarani au kushindwa kumudu kona.

Pia, alisema ukaguzi wa magari na madereva unaendelea kufanyika mara kwa mara na dereva anayebainika hana leseni halali au sifa zinazotakiwa anaweza kuzuiwa kuendesha hadi taratibu za kisheria zitakapokamilika.

Aliwataka wamiliki wa magari ya biashara kuhakikisha wanaajiri madereva wenye mafunzo na leseni zinazolingana na aina ya magari wanayoendesha ili kupunguza ajali zinazotokana na uzembe.

USULI >

## Takwimu za ajali za barabarani

**Serikali imesema watu 1,066 wamepoteza maisha kutokana na ajali za barabarani katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, ikiwa ni pungufu ya vifo 209 ikilinganishwa na watu 1,275 waliofariki katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25.**

**Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, alisema hayo bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/27.**

**Alisema matukio ya ajali za barabarani yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi nchini yamepungua kutoka ajali 1,322 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 hadi kufikia ajali 1,233 katika kipindi kama hicho mwaka 2025/26.**

**Aidha, alisema idadi ya majeruhi nayo imepungua kutoka watu 2,278 hadi 1,869, sawa na upungufu wa asilimia 18.42.**



# Ajali yaua watu sita Arusha

**Na LILIAN JOEL,** *Arusha*

WATU sita wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi la abiria na lori lenye tela barabara kuu ya Arusha-Dodoma, eneo la kijiji cha Naiti, Kata ya Makuyuni, wilayani Monduli, mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha Justine Masejo alisema ajali hiyo ilitokea jana saa 12.40 jioni, baada ya basi aina ya Higher lenye Namba za Usajili T 732 DRL, mali ya Kampuni ya Kandahari kugongana uso kwa uso na lori aina ya Howo lenye Namba T 727 EPW, lililokuwa limevuta tela Namba T 205 EPW.

"Katika ajali hiyo watu watano walifariki dunia papo hapo wakiwemo madereva, huku mtu mmoja akipoteza maisha wakati akipatiwa matibabu katika Kituo cha Afya Makuyuni," alisema.

Kwa mujibu wa Masejo, kati ya marehemu hao wanaume ni watatu na wanawake watatu, huku majeruhi wakiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Kamanda Masejo alisema uchunguzi unaendelea kubaini chanzo cha ajali hiyo, huku akitoa onyo kwa madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani, hususan kuyapita magari mengine katika maeneo yenye kona au yaliyowekewa alama za kukataza kufanya hivyo.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha hatutasita kuwachukulia hatua kali za kisheria madereva wote watakaobainika kukiuka sheria za usalama barabarani," alieleza na kusisitiza kuwa hakuna safari yenye umuhimu unaozidi thamani ya uhai wa binadamu.

Katika hatua nyingine, Kamanda Masejo aliwataka abiria na wananchi kwa ujumla kutotoa nafasi kwa uzembe wa madereva, bali watoe taarifa kwa vyombo vya usalama wanapoona dereva anaendesha chombo cha moto kwa mwendo kasi, kutokuwa makini maeneo hatarishi au anapokiuka sheria za barabarani, ili hatua zichukuliwe kabla ya kutokea kwa maafa.

Kwa mujibu wa mashuhuda, dereva wa basi alijaribu kulipita lori lililokuwa mbele yake katika eneo la kona kali bila kuchukua tahadhari lakini, kutokana na mwonekano hafifu wa barabara alijikuta akigongana uso kwa uso na lori lenye tela lililokuwa likitokea upande wa pili.

Mashuhuda hao walidai lori jingine lenye Namba T 757 DWV, lililokuwa likifuatana na semi-trela hilo, lilipinduka wakati dereva wake akifanya juhudi za kulikwepa eneo la ajali kuepusha kugongana na magari yaliyokuwa tayari yamehusika katika tukio hilo.